

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU
(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

MKOA WA MWANZA
Simu:- 028 – 2530002
FaxNo.:-028 – 2530199



Sanduku la Posta 200
MAGU.

Kumb. Na. MDC/Fs/L.120/III/31.

Tarehe: 17.05.2017

- Maafisa Uvuvi
- Makatibu wa BMU
- Watoza Ushuru mialoni.

YAH:- UHAKIKI WA WAVUVI, VYOMBO, LESENI ZA
UVUVI NA USHURU WA SAMAKI

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

1. Baada ya matokeo ya Sensa ya wavuvi na vyombo iliyofanyika mwezi Sept, 2016, imegundulika wavuvi wengi kutokuwa na leseni. Wavuvi hawa ni wale wanaotumia "mtindo" wa "Shift" au zamu, na wengine ni wale wanaotumia mazoea ya leseni za chombo kwa wavuvi watatu.
2. Ofisi itafanya zoezi la uhakiki wa kila mvuvi kwenye kila chombo muda mfupi ujao. Kila mvuvi anatakiwa kuwa na leseni yake wakati wote awapo kwenye shughuli za Uvuvi ndani ya maji (**ziwani**) na mwaloni.
3. Zoezi hili litahusisha pia ukaguzi wa ulipaji ushuru wa samaki kwenye mialo kwa wafanyabiashara na kwenye vyombo vya usafiri.
4. Watangazieni wadau wetu kuwa na leseni na vibali husika na kufuata taratibu zote za kisheria wakati wote ili kuepusha malalamiko na manung'uniko yasiyo ya lazima wakati wa zoezi.

Nawatakieni utekelezaji mwema.

AFISA UVUVI (W)
MAGU.

J.F.M. Mugarula,

AFISA UVUVI (W)
MAGU.

Nakala: Mkurugenzi Mtendaji (W),
Magu - Tunatekeleza agizo la CMT (15.5.2017)

: Mbao za matangazo maeneo ya mialo, masoko na vituo muhimu vya wavuvi.